

**MWANGAZA WA AKILI
YA BIKIRA MARIA NI
DIRA**



**Jinsi ya kufahamu nafasi ya Bikira Maria katika
ukristo**

HOSEA J.SIMWOGOPE


Mwandishi:
Hosea J.Simwogope.

Mawasiliano;
Barua pepe:hoseasimwogope@gmail.com.
WhatsApp:0758602036.
Instagram@Hosea Simwogope.
Facebook@Hosea Simwogope.

ISBN: 978-9912-40-117-4

Toleo la kwanza 2021

Imprimatur



Titus Mdoe
Askofu Jimbo Katoliki Mtwara

Kimechapishwa na

Truth Printing

0764 425 704/ 0692 637 282

geofreymakula@gmail.com

Dar es Salaam-Tanzania

DIBAJI



Ukiwauliza Wa-anglikana, mpo tayari kurudi katika Katoliki watakuuliza, ‘Je kama tukirudi tutapaswa kuamini mafundisho mawili msingi kwamba Bikira Maria alizaliwa pasipo dhambi ya asili na kwamba alipalizwa mbinguni?’

Ukiwauliza Walutheri na Jamii nyingine za Kikristo, ‘Mnamfahamuje Bikira Maria?’ Wao watakujibu ‘sisi tunajua hana nafasi yoyote katika wokovu wa mwanadamu, bali alikuwa tu kama bomba la kumpitisha Yesu.’

Ukiwauliza Waislamu, ‘Mnafahamuje Bikira Maria? Wao watakujibu, yeye (Mariamu) ni mama yake Issa (Yesu) ambaye alikuwa nabii mwenye vipawa vya hali ya juu.

Ukiwauliza Wakatoliki, Bikira Maria mnamfahamuje? Wao wana majibu mengi zaidi kulingana na wanavyoamini. Baadhi ya majibu hayo ni: Bikira Maria ni Mama wa Mungu, Alizaliwa pasipo dhambi ya asili, alipalizwa Mbinguni, ni Mama wa Kanisa, ni Mama yetu sote n.k.

Mwandishi wa Kitabu hiki, kwa namna ya pekee amemchambua Bikira Maria na nafasi yake katika Kanisa. Amejaribu kurejea Maandiko Matakatifu katika kumwelezea Bikira Maria na Uhusiano wake na Mungu-Mtu Yesu Kristo. Ameonyesha kwa karibu fadhila za Bikira Maria ambazo twapaswa kuziishi. Mwandishi amefanya marejeo pia katika

Mapokeo ya Kanisa na Mafundisho mengineyo ya Mama Kanisa kumhusu Bikira Maria.

Hata hivyo, mwandishi amemwelezea Bikira Maria kama mmojawapo wa waliookolewa na Yesu. Ikumbukwe kwamba, Yesu ndiye Mwokozi na njia pekee ya kutufikisha Mbinguni. Bikira Maria kamwe hachukui nafasi ya Yesu. Yeye hutuombea kwa Mwanaye, nasi twamsihi atuombea kwa Mwanaye; ambaye yuko karibu naye zaidi Mbinguni.

Kitabu hiki ni msaada mkubwa katika kumfahamu Bikira Maria na nafasi yake katika Kanisa Katoliki na wokovu wa mwanadamu kwa ujumla. Mkatoliki atakayesoma Kitabu hiki ataweza pia kutoa majibu kwa maswali mbalimbali kutoka dini na jamii nyinginezo za Kikristo kumhusu Bikira Maria. Ni kitabu cha aina yake kwa karne ya ishirini na moja; ambacho katika lugha ya Kiswahili kimerejea vyanzo vingi msingi kumhusu Bikira Maria.

Frt. Eugene Kawau (Jimbo Katoliki Moshi)

Mwanafunzi, Segerea Seminari – Dar es Salaam

Februari 23, 2021.

SHUKRANI



Napenda kumshukuru Mungu kwa zawadi ya uhai, akili, nguvu, afya, hekima, baraka, neema, na msaada katika kukamilisha mipango mbalimbali na yote ambayo Mungu ananijalia.

Napenda kuwashukuru wafuatao.

1. Uongozi wa Maktaba ya **“MTWARA REGIONAL LIBRARY”** na wafanyakazi wake wote kwa ushirikiano mzuri kwa muda wote niliokuwa natumia kuandika kitabu hiki.
2. Padre Victus Shemweta, kwa msaada alionipa katika kukipitia na kukamilisha kitabu hiki.
3. Padre Adam Bago; Kwa ushirikiano mzuri katika kukipitia kitabu hiki.
4. Padre Hubert Akweso; kwa ushirikiano mzuri katika kukipitia kitabu hiki.
5. Padre Faustin Mwikila Kamugisha, kwa ushirikiano na msaada katika kukamilisha kitabu hiki.
6. Jimmy Mahundi, Mwandishi wa habari; kwa kunipa maneno ya kutia moyo na hamasa pamoja na kukipitia kitabu hiki.

7. Padre Jerome, Mkurugenzi wa Shirika la Jesuit; kwa ushirikiano na kukipitia kitabu hiki.

8. Damian M.Ndimbo, Mwinjilisti, mwandishi wa mafundisho mbalimbali ya Imani katoliki kwa kukipitia kitabu hiki.

9. Tegemeo Patrick, Katibu Taifa TMCS; Kwa kukipitia kitabu hiki.

10. Mhashamu Askofu Titus Mdoe wa Jimbo la Katoliki la Mtwara kwa kukipitia na kwa kukipitisha kwa kupiga “IMPRIMATUR” na kuruhusu kitumike kukoleza utume wa Ufalme wa Mungu.

11. Wapendwa, Wazazi, Ndugu, Jamaa na Marafiki ambao wamenipa msaada na moyo wa kukamilisha kitabu hiki.

12. Kyuzeni Kambona, kwa ushirikiano wa laptop ambapo kazi hii ya kuandika pamoja na kukipangilia kitabu hiki katika nakala tete imefanyikia.

13. Kwako wewe ambaye unasoma kitabu hiki, Nakutakia usomaji mwema wa kitabu.

Kwa ujumla Napenda kuwashukuru wote walionisaidia katika kuandika na kukamilisha kitabu hiki kwa **USOMAJI, USAHIHISHAJI, USHAURI NA MAPENDEKEZO YAO KATIKA KUFANIKISHA KAZI HII.**

MWENYEZI MUNGU ATUBARIKI SOTE.

UTANGULIZI



Walatini wana msemu unaosema **“DESIDERIO DESIDRAVI”** ambao maana yake ni **“kwa nia ambayo nilinua”** katika maisha yangu, mojawapo ya kitu nilichokuwa napenda na ninachoendelea kupenda ni kuandika na kusoma vitabu mbalimbali vinavyogusa nyanja tofauti tofauti za maisha.

Hivyo nina furaha kubwa sana, kwa kukamilisha kitabu hiki chenye kuleta utume na mafundisho kuhusiana na Mama Bikira Maria.

Waswahili wana msemu unaosema **“MGAA GAA NA UPWA HALI WALI MKAVU”** Vile vile hata katika kusoma kitabu hiki utapata faida chungu nzima.

Kitabu hiki kinakupa tafakari ya kina kuhusiana na nafasi ya Mama Bikira Maria katika safari ya ukombozi wa mwanadamu na pia katika Ukristo. Na pia kitabu kinatuonyesha na kutuelimisha mambo mbalimbali yanayotusaidia kufikia usafi wa Roho zetu na kuwa na maisha ya utakatifu.

Walatini wana msemu unaosema **“MULTI MULTA SCIUNT, NEMO OMNIA”** Ambao maana yake ni **“WENGI WANAJUA MAMBO MENGI, LAKINI HAKUNA ANAYEJUA KILA KITU”** ,Hivyo hata kitabu hiki

kitakuongezea hekima mbalimbali za Mama Bikira Maria, ambaye ni Mama mwenye upendo mkubwa na dhati kwa dunia yetu ya leo.

Katika mkabala huo, kitabu hiki ni chachu ya kutukumbusha nafasi ya Mama Bikira Maria na hasa katika kipindi hiki ambapo kina utitiri wa madhehebu, dini, imani na makanisa mapya kila uchao.

Kwa watu wanaochimba madini, hupitia uzoefu huu, mwanzoni wanapoanza kuchimba madini wakati ambapo mgodi unakuwa bado mpya, madini huwa yapo karibu karibu na hivyo wanaochimba madini katika kipindi hiki hupata madini kwa urahisi na bila kwenda kina cha mbali.

Lakini kadiri madini yanavyopatikana na kadiri mgodi unavyochimbwa, ndivyo hufikia wakati ili uyapate madini unatakiwa uchimbe chini zaidi ndipo uyapate madini.

Vile vile kitabu kinatufundisha kwa mfano wa Mama Bikira Maria kwamba ili tuweze kufikia mafanikio ya **KIROHO**, Sio kazi lelemama, Mama Bikira Maria alipitia mengi na magumu na akawa na jicho la tatu la kutazama mafanikio ya Kiroho, Hivyo tutafakari kwa makini hekima za kiteolojia, Kiroho na kiliturujia na tuyatoe na kuishi maisha yetu kwa matendo ya kila siku yanayotupelekea kufikia utakatifu na usafi wa Roho.

Nawatakia usomaji mwema wa kitabu.


Na **MWANDISHI WA KITABU,**

HOSEA JUSTINE SIMWOGOPE NGONGOGE


SIMU: 0758602036 / 0710375563.

Barua pepe:hoseasimwogope@gmail.com

Facebook@Hosea Simwogope. 

Instagram@Hosea Simwogope. 

Youtube link:https://youtu.be/7ETr_bgcdNs 

Whatsapp Number;0758602036 

YALIYOMO	
DIBAJI	3
SHUKRANI	5
UTANGULIZI	7
SURA YA KWANZA;	12
MAMA BIKIRA MARIA NI NANI.....	12
TUSOME SEHEMU ZIFUATAZO ZA BIBLIA TUONE MUNGU ALIVYOMCHAGUA NA KUMPA HADHI MAMA BIKIRA MARIA.	16
MAANDIKO YANAYOSHUHUDIA UMUHIMU WA WATU UNATOFAUTIANA	20
SURA YA PILI;	23
BIKIRA MARIA KATIKA BIBLIA.	23
SURA YA TATU;	49
DOGMA ZA KANISA KUHUSU BIKIRA MARIA.....	49
1. MKINGIWA DHAMBI YA ASILI	49
SURA YA NNE;	57
MAMBO KUMI TUNAYOJIFUNZA KUTOKA KWA MAMA BIKIRA MARIA NA TUNAHITAJI TUYAISHI KATIKA MAISHA YETU KWA MATENDO.	57
1. IMANI THABITI KWA MUNGU.	57
2. TUWE NA UKARIMU KWA WENZETU.....	64
3. TUWE WANYENYEKEVU.	68

4. KUJITOLEA KWA AJILI YA MUNGU.	71
5.TUWE WAVUMILIVU.	74
6.MATESO YANA NAFASI KATIKA MAISHA.	75
7.TUKUZE, KUCHOCHEA NA KUONGEZA WITO WA UPADRE.....	81
8.TWENDE KUUNGAMA KWA WOKOVU WA ROHO ZETU.	84
9. TUISHI UMUNGU WA MUNGU KWA MATENDO.....	97
10. TUWE NA UPENDO UNAOTEKELEZEKA KWA MATENDO.....	103
SURA YA TANO;	113
HESHIMA ZA LITURUJIA KWA MARIA NA DHAMIRA ZA KANISA KATOLIKI ZA SIKU NA KIMWEZI.....	113
1. SHEREHE	113
2. SIKUKUU	114
3. KUMBUKUMBU	114
4. KUMBUKUMBU YA HIARI.	114
5. KANISA KATOLIKI NA DHAMIRA ZAKE.	114
A.DHAMIRA ZA KIMWEZI.....	114
B.DHAMIRA ZA SIKU.	115
6. JE, TUNAMUABUDU BIKIRA MARIA?	116
MAREJEO	118

**SURA YA KWANZA;
MAMA BIKIRA MARIA NI NANI.**



“Ishi kwa furaha ukiwa na Maria;Yavumilie masumbuko yako yote ukiwa na Maria;Fanya Kazi pamoja na Maria;Sali pamoja na Maria;Nenda kupumzika pamoja na Maria;Ukiwa na Maria nenda kulala.Mtafute Yesu ukiwa na Maria;Mbebe mikononi mwako Yesu,Nawe pamoja na Yesu na Maria weka makao yako huko Nazareti.Nenda Yerusalemu ukiwa na Maria,Kaa karibu na Msalaba wa Yesu,Jizike mwenyewe pamoja na Yesu.Ukiwa na Yesu na Maria fufuka tena,Pamoja na Yesu na Maria paa mbinguni,Ishi na kufa ukiwa na Yesu na Maria.”

Thomas A.Kempis.







Mama Bikira Maria alizaliwa na Watakatifu Yoakim na Ana. Ambapo Yoakimu maana yake “Mungu anaokoa na Ana maana yake “Neema”. Familia ya Mama Bikira Maria iliishi Nazareth. Mama Bikira Maria ndiye aliyemzaa Yesu Kristo, Mkombozi. Jina Yesu linatokea kwenye neno la Kiebrania “YESHUA” neno lenye maana ya “WOKOVU”. (Mt. 1; 21-25 na Lk 1; 31). Tuelewe Wokovu ni Yesu. Mama Bikira Maria alianza maisha yake kwa kupata heri ya pekee, Mungu alimkinga Mama Bikira Maria na dhambi ya asili kusudi awe Mama wa Mkombozi. Kila mtu amezaliwa na dhambi ya asili, na Sakramenti ya Ubatizo ndiyo yenye nguvu ya kuondoa dhambi ya asili. Hivyo ni jambo ambalo lipo wazi, Tusipopata ubatizo, Tutakufa na dhambi ya asili. Yesu alitangaza kuwa Mama Bikira Maria Ndiyo Mama Yetu, Pale Msalabani alimwambia Mtakatifu Yohane.

TUSOME SEHEMU ZIFUATAZO ZA BIBLIA TUONE MUNGU ALIVYOMCHAGUA NA KUMPA HADHI MAMA BIKIRA MARIA.

LUKA 1;38 “Maria akasema, Mimi ni mtumishi wa Bwana,nitendewe kama ulivyosema,Kisha Yule Mwanamke akaenda zake”.

ISAYA 7;14 “Haya basi,Bwana mwenyewe atawapa ishara; Tazama Bikira atachukua mimba, Atazaa mtoto Mwanaume, Naye atamuita jina lake Emanueli,Yaani Mungu pamoja nasi”.

LUKA 1;28-31 “Malaika akamwendea, akamwambia, Salamu, Ewe uliyeneemeshwa na Mungu. Bwana yuko nawe.Maria aliposikia maneno hayo alifadhaika sana, Akawaza maneno hayo yanamaanisha nini? Malaika akamwambia, Usiogope Maria, Kwa maana Mungu amekujalia neema. Utachukua mimba, Utamzaa mtoto wa kiume, Nawe utampa jina Yesu”.

Kutangazwa kwa uzazi wa Yesu kulizindua wakati ule maalum wa kutimizwa kwa ahadi na matayarisho ya Mungu katika historia ya Ukombozi wa Wanadamu. Maria aliteuliwa na Mungu tangu milele awe Mama wa Yeye ambaye ndani yake mna utimilifu wote wa Mungu (Kol 1;19).

Maria alikuwamo katika mawazo na mpango wa Mungu tangu milele. Mtakatifu Louis wa Montfort alisema kwamba “Mungu alipofanya kazi ya uumbaji, Alikusanya maji akayaita bahari, kwa kilatini “Mare”. Mtakatifu huyu alisema pia”Mungu huyo huyo alikusanya neema zake na kuziita Maria,kwa kilatini “Maria” maana yake bahari nyingi.

Mungu alimchagua mtu mmoja jina lake Yosefu, Mwana wa Daudi, Ambaye alikuwa mwadilifu kuwa mume wake Maria na Baba Mlishi wa Mwanawe. Adamu wa Kwanza alitoka kwa Mungu bila njia ya Mwanamke; Adamu wa pili, Yesu Kristo, Alitoka kwa Mungu bila njia ya Mwanaume. Mwana wa Mungu ambaye ana Baba wa milele mbinguni, Hakuhitaji kuwa na Baba hapa duniani. Lakini yeye ambaye hakuwa na Mama mbinguni, ilifaa awe na mama hapa duniani. Kwa sababu hiyo, Mwana wa Mungu” Alitungwa kwa Roho Mtakatifu”. Akazaliwa na Bikira Maria. Kama Mungu aliweza kuumba Mbingu na dunia kwa neno lake tu, Je angeshindwa kumfanya Yesu azaliwe duniani kwa namna anavyoona mwenyewe inafaa?

Mungu anaweza yote, kwake hakuna lisilowezekana. Maria mwenyewe kwa imani kubwa, Akitambua na Kukiri uwezo huo wa Mungu alisema;” Mimi ni mtumishi wa Bwana, Nitendewe kama ulivyosema” Luka 1;38.

Kwa wale wasiotembea pamoja na Mama Bikira Maria, Twatumia maneno haya ya Mtakatifu Augustino;”Bene Curris Sed Extra Viam” ; Maana yake “Unakimbia vizuri lakini umepotea njia, Utafika wapi mwisho.”

Maria alimzaa Yesu Betlehemu ambako alikuwa ameelekea pamoja na Yosefu kwa ajili ya sensa. Mengi aliyooona na hasa kusikia, Wachungaji walipokuja kumtazama, Aliyaweka na kuyatafakari moyoni mwake.

Mama Bikira Maria alizaliwa tarehe 8 Septemba. Kumbukumbu hiyo imeadhimishwa tangu karne ya 5, Lakini hata tangu karne ya 2 mapokeo ya kikristo yametaja majina ya

wazazi wake kuwa Yoakimu na Ana.Ibada kwa heshima ya Mtakatifu Ana ilianza karne ya 6, Na ya kumheshimu Mtakatifu Yoakimu ilianza muda mrefu baadaye, Yaani karne ya 16.

Kutolewa kwake Hekaluni Bikira Maria ni tarehe 21 Novemba.Mapokeo ni kwamba chini ya Uongozi wa Roho Mtakatifu, Maria tangu utoto wake alijiweka mikononi mwa Mungu.Kadiri ya mapokeo mengine, Maria aliletwa Hekaluni, Akatolewa kwa utumishi wa Bwana Mungu.Mtakatifu Bernado alisema” Maria alimpendeza Mungu kwa Ubikira wake, Lakini alichukua mimba kwa unyenyekevu wake”. Unyenyekevu umejengwa juu ya upendo. Ndiyo maana Bwana wetu Yesu kristo alisema “Mkinipenda mtazishika amri zangu”.

Bikira Maria alimpenda Mungu. Ni kwa upendo huu alikuwa tayari kunyenyekea na kuchukua mimba ya Mkombozi. Hatuna budi kujinyenyekeza mbele za Bwana. Unyenyekevu ni mama wa fadhila nyingi kama ifuatavyo;

- I. Utii
- II. Uchaji
- III. Ibada
- IV. Uvumilivu
- V. Kiasi
- VI. Upole na
- VII. Amani

Mtakatifu Thomas wa Killanova alisema “Yeye ambaye ni mnyenyekevu hutii kila mtu, ni mwema kwa wote, ni mtiifu kwa kila mtu, hamchukizi wala kumuudhi yeyote”

Kinyume na unyenyekevu ni majivuno. Majivuno ni kilema hatari sana. Mwenye majivuno hufikiri ameshafika kwenye kikomo cha safari. Na mnyenyekevu hujua kuwa duniani tu wageni, duniani tu wasafiri, mambo bado. Majivuno ni kilema hatari sana.

Mtakatifu Augustino alisema “Majivuno yaliwabadili malaika wakawa mashetani. Unyenyekevu huwafanya watu kuwa malaika” Mama Bikira Maria ni mfano wa kuigwa katika unyenyekevu.

Safari zote za binaadamu zinaanza na “moyo”. Tamaa zote za mwili zinaanza “moyoni”, ila moyo wa binadamu ni chungu cha sala. Kama Mama Bikira Maria alivyotusisitizia, kwa sababu huwezi kuishi kwa kutumikia mabwana wawili (You can’t live double life). Mungu ametupa upendo tusaidiane.

Penye neema pana mateso, na kwenye mateso kuna neema. Bikira Maria ni bikira, ubikira wake una imani yake. Kama tunavyosoma katika 1 Wakorintho 7:34-35 “Naye amegawanyika, mwanamke asiyeolewa au bikira hujishughulisha na mambo ya Bwana apate kujitolea mwili na roho kwa Bwana. Lakini mwanamke aliyeolewa hujishughulisha na mambo ya dunia hii atakavyompendeza mumewe. Ninawaambieni haya kwa faida yenu, na si kwa kuwawekeeni kizuizi. Nataka tu muwe na mpango unaofaa, mpate kumtumikia Bwana kwa moyo na nia moja”.

Hivyo Mama Bikira Maria alinyima anasa, kwa sababu ya kumpenda Mungu. Lakini vijana katika dunia ya leo tunapenda “Taste” Na watu hawataki kutumia roho zao na kutafakari mambo, badala yake watu wanatumia macho.

Kwa utii wake Bikira Maria amekuwa Eva mpya, tumuheshimu Bikira Maria, ni Mama wa Yesu. Tusiwe na haraka ya maisha, tuwe wavumilivu (Let us be patient).

Bikira Maria alimpendeza Mungu kwa unyenyekevu wake kama Mtakatifu Ambrosi Anavyotuambia “Oneni unyenyekevu gani; anajiita mwenyewe mtumishi wa Mungu saa ileile naye anapochaguliwa naye awe mama mzazi wa mungu mwana. Anapashwa habari habari atakuwa mkubwa ajabu, lakini hapati majivuno hata kidogo.

MAANDIKO YANAYOSHUHUDIA UMUHIMU WA WATU UNATOFAUTIANA

Maandiko matakatifu yanawasifu watu mbalimbali kutokana na walivyomwamini Mungu na kutenda makuu kwa ajili ya taifa lake.

Kuna msemu mmoja mzuri sana wa kilatini unaosema “UBI CARITAS ET AMOR DEUS IBIEST” ambaye maana yake ni “Mahali palipo na amani na upendo Mungu yupo”. Tuangalie watu mbalimbali waliokuwa na upendo na amani kutokana na walivyomuamini Mungu na kutenda makuu

1. Abrahamu alimwamini Mungu na kuwa tayari kumtolea Mungu sadaka mwana wake Isaka, tukio lilimfanya apate baraka ya pekee ya kuwa baba wa waamini (Mwanzo 22:15-18), Abrahamu alikuwa na upendo, imani ya kweli, mnyenyekevu, mskivu, mvumilivu na aliyekuwa na hofu ya Mungu. Abraham is called “Father of Belief” (Baba wa Imani)

2. Yosefu, kipenzi cha Yakobo, alikuwa mwaminifu hata aliokoa taifa lisiangamie na njaa (Mwanzo 50:20) na alikuwa na kipaji kizuri cha kutafsiri ndoto, unadhani ni hali ya kawaida yote hayo ni kwa sababu alikuwa mwaminifu kwa Mungu, ndivyo anashushiwa Baraka na neema mbalimbali.
3. Musa, ndiye mkombozi wa taifa la Mungu katika Agano la kale: aliongoza Israeli kutoka utumwani Misri, akalipatia sheria kutoka kwa Mungu katika mlima Sinai. Maandiko ya kale yanakiri “Wala hajainuka kiongozi kama alivyokuwa Musa” (Kumb 34:10-12)
4. Yoshua
5. Debora
6. Gideoni
7. Samsoni
8. Samweli
9. Ruthu
10. Wafalme, Daudi na Solomoni
11. Manabii Eliya, Yeremia na Ezekieli
12. Nabii Isaya ana sifa ya pekee katika kumchora Masiya
13. Mwishoni Bwana Yesu mwenyewe anamsifu Yohana Mbatizaji akisema (Luka 7:24-28).

Bikira Maria ana nafasi gani kati yao?

Hao tuliowataja kweli mambo makuu kwa imani, lakini Bikira Maria yuko juu sana kupita hao wote, tena kwa mbali: yeye ni malkia wa makundi yote ya mbinguni, sio watu tu, bali hata

ya malaika. Mapokeo ya mashariki humuita “daraja linalounganisha dunia na mbingu” mfano aliouona Yakobo (Mwa 28:12).